

Jinsi COVID-19 Inavyosambaa katika Jamii

Si watu wote walio na COVID-19 huhisi wanaugua. Lakini hata kama wanajihisi wazima, bado wanaweza kuwaambukiza watu wengine.

Mtu aliye na COVID-19 akienda kwenye harusi, mazishi au kwenye mkusanyiko mwingine wowote mkubwa wa watu, anaweza kuwaambukiza virusi watu wengine waliopo. Hili linaweza kufanyika hasa ikiwa watu hawavai barakoa, na ikiwa hawakai angalau futi 6 mbali na wengine.

Watu wengine wanaoambukizwa kwenye hafla hiyo kisha watasambaza virusi hivi nyumbani kwa familia na marafiki zao. Ikiwa wanaishi nje ya mji, watasambaza COVID-19 huko pia.

Kila mtu anayeishi naye sasa ataambukizwa. Na ikiwa watu wote wataenda kazini, shuleni au mahali pengine popote ambapo watu hukusanyika, watu walioko hapo wanaweza kuambukizwa pia.

Hatua inayoanza kama mtu mmoja aliye na COVID-19 inaweza kuwa maambukizi ya watu kadhaa, isipokuwa watu wakichukua hatua ya kuzuia kuenea kwa virusi hivi.

Chukua hatua za kulinda familia, marafiki na watu ambao huenda hata huwajui.

Usiende kwenye mkusanyiko mkubwa wa watu.

Vaa barakoa.

Kaa angalau futi 6 mbali na wengine.

Nawa mikono yako.

Na ukae nyumbani ikiwa unahisi kuugua.

Minnesota Department of Health
Communications Office
PO Box 64975
St. Paul, MN 55164-0975
651-201-4989
health.communications@state.mn.us
www.health.state.mn.us

20/10/20 (Swahili)

Ili upate maelezo haya kwa muundo tofauti, piga simu: 651-201-4989